**African Entrepreneurs – Successful and Responsible**

**Episode: 3**

**Titel: A fresh business vision – Sydney Tumelo Mokheti's Black Apple Consulting in South Africa**

**Author: Leonie March**

**Editors: Katrin Ogunsade, Adrian Kriesch**

**Proofreading: Natalie Glanville-Wallis**

**Kisuaheli:Eric Ponda**

**Characters (O-Töne, Clips) / Narrators**

| | Women | Men | Age | Language |
|---|---|---|---|---|
| Intro/Outro | | x | Unimportant | |
| Narrator | x | | Unimportant | |
| Sydney Tumelo Mokheti (clip) | | x | 27 | English (high voice) |
| Thabo Radebe (clip) | | x | 27 | English |

**Pronunciation:**

Sydney Tumelo Mokheti (pronounced as written)

Roodepoort (pronounced: Rodeport)

Bloemfontein (pronounced: Bloomfonteyn)

Thabo Radebe (pronounced as written, German "e")

CIDA (pronounced as word)

**Intro:**

Hujambo na karibu kwa makala nyingine ya "Learning By Ear", Noa Bongo Jenga Maisha yako tikuwa bado tunaswaangazia wajasirimali chipukizi barani Africa ambao wamefanikiwa katika biashara zao na kuchangia katika kubadilisha maisha yaw wengine miongoni mwa jamii wanamoishi. Kipindi cha leo tunafunga safari hadi mji mkuu wa Africa Kusini Johannesburg ambako tunakutana na mfanyi biashara Sydney Tumelo Mokheti. Yeye ni muasisi na mkurugenzi mkuu wa kampuni ya Black Apple Consuting inayotoa usahuri na huduma za teknolojia ya mawasiliano

1. ***Sound: School***

2. ***Narrator:***

Siku hizi Shule ndio wateja wakuu wa kazi hii ninayofanya anasema Sydney Tumelo, akitembea katika vinjia vya majengo ya shule moja ya sekondari mjini Johannesburg, huku akiwasalimia waalimu wa shule hiyo kwa tabasamu. Akiwa amevalia suruali ya Jean na shati la mikono mirefu,kila mmoja anampenda kijana huyu mwenye umri wa miaka 27 ambaye anatangamana na watu kwa urahisi. Na huku akitabasamu anakumbuka enzi zake alipokuwa bado shuleni.

3. ***Sydney:***

"Nikiwa na umri wa miaka 6 niligundua kipawa changu kwamba ningetaka kuwa mfanyi biashara. Nimekuwa na uchu wa kufanya biashara. Enzi hizo nilikuwa nikizunguka shuleni nikiuza peremende baada ya masomo. Na hivyo nilijia kwamba naweza kuwa mfanyi biashara mzuri."

4. ***Narrator:***

Mfanyi biashara huyo anachunguliwa ofisi ya sekretari wa shule hiyo kisha kubisha hodi na kupita ndani.

5. *Sound: conversation with secretary*

6. ***Narrator:***

Baada ya makaribisho moto moto na busu kutoka kwa sekretari huyo, Sydney anataka kujua jinsi mitambo mipya ya Komputa iliyowekwa na kampuni yake  wiki mbili zilizopita bado inafanya kazi vizuri. Na anaambiwa mambo ni shuari kabisa. Ila tub ado wafanyi kazi hawajaanza kufungua Email zao. Sydney anaitikia na kumuaga sekretari huyo.

7. ***Sound: Street***

8. ***Narrator:***

Baada ya muda wa saa moja na nusu katika ofisi za shule hiyo Sydney anarudi ofisini mwake zilizoko mtaa wa Roodepoort kitongoji cha mji huo wa Johannesburgh kinachozungukwa na migodi ya dhahabu. Ofisi zake zinaonekena zisizo na mpangilio wowote kinyume kabisa na linavyoashiria jina la kampuni hiyo Black Apple Consulting. Wachuuzi wamepanga mali zao hadi kwenye lango la ofisi hizo zinazopakana na Benki, osifi za mganga wa kienye na hata ukumbi wa huduma za intaneti

9. ***Sound: Black Apple office***

***10. Narrator:***

Sydney anaingia ofisini mwake yenye shughuli nyingi ,vijana na wasichana wakiwa wanafanya kazi zao katika komputa zao huku wakishauriana kwa sauti ya chini. Sydney ndio mkubwa au kama inavyofahamika mkurugenzi mkuu wa kampuni hii. "Na hawa ni wafanyakazi wangu," anatufahamisha. Vijana hao wanang'ang'ana kubuni ukurasa wa tmtandaoni na chapa cha kampuni hiyo kuelezea kwa urahisi malengo ya kampuni hiyo, mwito na nembo ya kampuni hiyo. Lakini hii ni baadhi ya shughuli nyingi za kampuni hiyo.

***11. Sydney:***

"Pale tuna idara inayohusika na utaalam wa teknolojia ya mawasilian. Maafisa wa idara hiyo ndio wanaohusika na kuweka mitambo ya Komputa, kurahisisha na kusambaza teknolojia hii ya mawasiliano,kazi ambayo mimi binafsi ninayoipenda sana. Na ndio msingi wa shughuli za kampuni hii."

***12. Narrator:***

Sydney Mokhetti anakalia kiti chake cha sofa karibu na mlango wa ofisi yake, ni kiti cha aina yake na cha stareje kilichoundwa kwa mtindo wa kisasa kabisa katika ofisi hiyo. Biashara hii ni kama ndoto tu anasema Sydney anapoanza kutueleza historia ya biashara yake. Sydney alizaliwa na kulelelewa katika mji wa Bloemfontein, mdogo zaidi

ukilinganishwa na mji wa Johannesburgh. Hakuna mtu aliyefikiria kuanzisha biashara kama hii. Anasema Sydney.

***13. Sydney:***

"Nadhani changamoto kubwa ambayo nimekuwa nayo ni nani anayeweza kukuza na kuendeleza kipawa hicho changu? Sababu mara nyingi njia za kutafuta pesa zinachanga moto zake na ni rahisi Mtu kujikuta unatumbukia katika mambo mapya ambayo yanaweza kukuharibu maishani. Ni jambo geni sana kwetu sisi kuwa mfanyi biashara aliyefaulu na kuanzisha kampuni kubwa ya kimataifa. Na hivyo ndio changamoto inayonikabili."

***14. Narrator:***

Lakini kijana huyu aliweza kufuatilia na kutimiza malengo yake. Kwanza alipita mitihani yake shuleni ambako alifana vyema zaidi katika somo la hesabu na masuala ya biashaa. Alikuwa mionmgoni mwa wanafunzi bora zaidi na kupata msaada wa masomo katika chuo kikuu cha CIDA, mjini Johannesburg, chuo kinachowasaidia watoto kutoka jamii maskini kuendeleza masomo bila malipo.

***15. Sound: Black Apple office***

***16. Narrator:***

Na ni katika chuo hiki ambako Sydney alikutana na Thabo Radebe, rafiki yake wa rika moja ambao walikuwa na maono sawa maishani. Vijana hao walishirikiana baada ya kumaliza chuo kikuu katika kuanzisha kampuni hii ya Teknolojia ya mawasiliana, masuala ya uuzaji na usimamizi ya Black Apple. Lakini cha kushangaza ni kwamba tabia zao

ni tofauti kabisa. Sydney hupenda sana kuzungumza, na mwenye kutangamana kwa urahisi za watu, Thabo ni mkimya asiyependa kimbelembele.

***17. Thabo:***

“Ningependa kuwashauri wengine kwamba wakati unapoanzisha biashara na rafiki yako lazima mkubaliane katika masuala kadhaa kwa lengo la kusaidiana na wala sio kushindana.Mfano tuliposhikana na rafiki yangu Sydney tulikubaliana kwamba yeye awe mkurugenzi mkuu kwa sababu yeye anapenda sana kuzungumza na ni Mtu wa watu hivyo nikamwambia achukue wadhifa wa Mkurugenzi mkuu, lakini kama sote tungekuwa tuning’ang’ania wadhifa huo, basi mambo yangeenda mrama.Mimi husimamia kazi za ofisini na kupanga kazi za kila siku ofisini kuhakikisha kuwa  kila mfanyi kazi anafanya kazi yake ipasavyo. Nadhani huo ndio msingi wa uhusiano wa kibiashara kwasababu kila mmoja anafahamu vyema majukumu yake.”

***18. Narrator:***

Vijana hawa waliovuzu chuo kikuu, walianza biashara yao bila ya kuwa na pesa za kutosha. Tulianzisha biashara hii katika jingo moja tulilokluwa tukitumia kwa pamoja wakati huo, anakumbuka jisnsi walivyokuwa wakitumia chumba kimoja na Sydney kama ofisi.

***19. Thabo:***

“Tulijaribu kutafuta pesa, lakini hakuna tasisi yoyote ya serikali au benki ilikuwa tayari kutusaidia.Kama unavyofahamu, huwezi kupata mkopo kwa urahisi kutoka benki kutokana na masharti magumu na kadhalika…Na tukaamua kwamba muhimu ni msaada.. Msaada kutoka kwa marafiki, familia na kadhalika. Na ndipo tulipokuwa pamoja

kuhakikisha kunapata msaada huo kwani hiyo ndio iliyokuwa njia pekee mfano akitoa nusu 250 nami nikitua nusu 250 ni 500 na tunaweza kuanzisha biashara. Hivyo ndivyo tulivyoanza."

***20. Narrator:***

Kufikia sasa wawili hao wameweza kuwaajiri wafanyi kazi 12. Mara nyingine kazi inakuwa nyingi mapaka unashikwa na kisunzi kutokana na majukumu mengi anasema Sydney.

***21. Sydney:***

"Siwezi kukudanganya, hapa kazi ni nyingi sana mpaka unaweza kutokwa na wazimu. Umuazi unaoanya unamuathiri Mteja, unawaathiri wafanyi kazi,unaathiri mishahara yao na pia kuna madeni yanapasa kulipwa. Hivyo ni muhimu kuwa na mpangilio bora zaidi na kubadili utaratibu wa utendaji kazi ili kusiwepo na tatizo. Na njia moja ya kufanya hivyo ni kutoa majukumu kwa watu wengine, Mimi na Thabo tunasimamia idara ya utaalam wa teknolojia,uuzaji usimamzi wa kazi za ofisini huku tukitoa majukumu mengine wa wafanyi kazi. Si kama zamani ambapo tulikuwa tukifanya kila siku.Lazima kuwepo na mabadiliko ya mtazamo wa kibiashara na mbinu za usimamizi pia ili kumpa fursa kila mmoja kufanya kazi yake,ndio kampuni hii imeweze kunanuka zaidi."

***22. Sound: Black Apple office***

***23. Narrator:***

Biashara imeimarika sasa lakini mwito wao bado ni ule ule. Wamejitolea kuwasaidia wengine kwa kuandaa warsha kuwahamasisha vijana

kushirikiana na wataalam katika kukuza vipawa vyao, kutoa misaada ya komputa kwa shule zilizoko sehemu zinazokumba hali ya umaskini mbali na kuwasadia vijana kuanzisha biashara zao, anasema Thabo Radebe.

***24. Thabo:***

"Mfano mtu akija na wazo la biashara na hana njia za kupata ufadhili, na tukiona ni wazo zuri, tunamsaidia kifedha kuanzisha biashara hiyo kwa faida kidogo. Tunataka kuvunja ukiritimba  na masharti yanayotolewa na taasisi za kifedha, kwasababu watu wengi wanamawazo mazuri sana ya kibiashara lakini tatizo ni ufadhili. Washindwa hata kumudu huduma za intaneti au kununua kompyuta.".

***25. Narrator:***

Sydney anafurahi wakati Mwenzake anapozungumza. Anakumbuka walikotoka, na jinsi biashara yao ilivyobadilisha maisha yao.

***26. Sydney:***

"Kila wakati naota kuhusu biashara jambo ambalo halikuwahi kufanyika siku za mbeleni. Nilikuwa nikitamani kuendesha magari, na kufanya starehe na marafiki zangu. Lakini sasa kwasababu biashara inaimarika kwa haraka, nasikia uzito wa jukumu linalonikabili na sasa na waza kila wakati na hata mara nyingi nikiwa usingizini ambapo huambka na kuandika chini yale yote yaliyonikujia kwenye ndoto kuhusu biashara. Kisha wakati ninapowasilisha wazo hilo kwa wenzangu, ndipo unappofahamu kwamba lilikuwa wazo la busara lenya kukuletea pato la mamilioni ya randi. Na ni jambo la kufurahisha kuona wenzako wakikuunga mkono na kupenda wazo lako."

***27. Narrator:***

Mwanzoni Thabo alikuwa msumbufu sana na haikuwa rahisi kumshawishi Kila mara alikuwa akishuku wazo la Sydeny kuona kama linaweza kuwaletea mamilioni ya Randi za Afrika Kusini ndipo aweze kulikumbatia.

***28. Thabo:***

Mimi husema tusijidanganye, hebu tulijaribu kama wazo lako linaweza kufaulu. Tunajaribu kulichambua na mimi hufurahi kama wazo hilo linapofaulu. Lakini anapoona kuwa halifai anarudi nyuma. Hii si ndoto tena lazima tuhakikishe kuwa si mambo ya kubahatisha (laughs) siku hizi lazima tuchambua kila wazo jipya kwa kina sana."

***29. Narrator:***

Ni jambo la kufurahisha kuzungumza na vijana hawa wawili washirika wa kibiashara ambao huonekana kuchukulia mzaha mambo wanayofanya, ingawa wanasimamia kampuni muhimu inayohitaji ujuzi na ufahamu wa hali ya juu. Hata hivyo lakini furaha yao kubwa ni kutoa msaada wa ushauri kwa vijana wanaotaka kuiga mfano wao.

***30. Thabo:***

"Ningependa kuwahimiza vijana  hasa kutoka mataifa barani Africa kushirikianaKwani hiyo ndio njia pekee ya kupata ufanisi. Mfano watu 5, 6,7 au 8 wakija pamoja na kushirikiana inakuwa rahisi sana. Iwapo tutafanya hivyo basi tunaweza kupiga hatua kubwa sana kwasababu imekuwa vigumu na bado ni vigumu sana kupata mikopo kutoka kwa taasisi za kifedha."

***31. Narrator:***

Sydney anakubaliana n a wazo hilo. Anaamini kuwa njia pekee ya kupata ufanisi ni kupitia ushirikiano.

***32. Sydney:***

"Nakumbuka nikiwa chuo kikuu cha CIDA tulikuwa na msemo kwamba ni Inataka moyo kwa kijana kulea kijiji.Inataka moyo kusambaza habari kwa lengo la kuendeleza kijiji kizima. Hivyo ni muhimu kushirikiana kusambaza habari kama kitu kimoja, na kuwa na hamu ya kutaka kujua , ni vipi, na kwanini na mambo yanavyokwenda. Ni muhimu kujifunza kila wakati, unajifunza kutokana na mazingira uliyomo, unajifunza kutokana na tajiriba, kutangamana na watu shuleni na kadhalika. Unahakikisha kuwa kila jambo linaandamana nay ale unayotaka kufanya maishani."

**<u>Outro:</u>**

Sydney Tumelo Mokheti, tunakushukuru sana kwa muda wako kutufahamisha mengi kuhusu biashara na matumaini yako siku za usoni. Tukiamini wewe msikilizaji pia umejifunza mengi na kufufahia kipindi hiki cha Learning By Ear Noa Bongo jenga maisha yako.Mwandishi wetu alikuwa Leonie March. Iwapo ungependa kukusikiliza tena kipindi hiki au kutuma maoni, tembelea mtandao wetu wa www.dw.de/lbe. Hadi wakati mwengine tena tutakapoungana nawe kwa kipindi kingine cha NOA BONGO, Kwaheri kwa sasa.